# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

## KIKAO CHA PILI

**28 AGOSTI, 2024**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

## KIKAO CHA PILI – TAREHE 28 AGOSTI, 2024

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA UCHUKUZI:**

Maelezo ya Waziri wa Uchukuzi kuhusu Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka 2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka 2024.

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**21. MHESHIMIWA ROSE VICENT BUSIGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Nhomolwa - Mbogwe.

**22. MHESHIMIWA ALLY JUMA MAKOA (KONDOA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka fedha za ujenzi wa uzio wa Shule ya Wasichana Kondoa ili kuimarisha ulinzi na usalama wa Wanafunzi.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**23. MHESHIMIWA NG'WASI DAMAS KAMANI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza ustawi wa familia kwa kuweka Wanandoa Waajiriwa katika Vituo vya Kazi vya jirani.

**WIZARA YA NISHATI:**

**24. MHESHIMIWA SOUD MOHAMMED JUMAH (DONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuharakisha Miradi ya LNG nchini ili kuchochea uchumi na kupunguza matumizi makubwa ya kuni na mkaa.

**WIZARA YA FEDHA:**

**25. MHESHIMIWA ZAHOR MOHAMMED HAJI (MWERA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, lini Serikali itaondoa mzigo wa kodi kwa Vyombo vya Ulinzi na Usalama nchini.

**26. MHESHIMIWA JESCA JONATHANI MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, ni muda gani Hazina hulipa malipo ya katikati ya mwezi kwa Wastaafu kwa Mfuko ulioanza mwaka 1992 kwa kuwa hawalipwi kwa wakati.

**27. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuelekeza Benki za CRDB, NBC na NMB kufungua Matawi eneo la Kikatiti linalokua kwa kasi.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**28. MHESHIMIWA PROF. PATRICK ALOIS NDAKIDEMI (MOSHI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali imechukua hatua gani za muda mfupi wa kati na muda mrefu kunusuru theluji inayotoweka Mlima Kilimanjaro.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**29. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itajenga jengo la kisasa la Mahakama Wilaya ya Meatu.

**WIZARA YA KILIMO:**

**30. MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MASWA MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kuna ushindani miongoni mwa Wafanyabiashara na Wanunuzi wa Zao la Pamba nchini.

**31. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA (ULYANKULU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni sababu zipi zinasababisha Wakulima wa Tumbaku kukopeshwa pembejeo na kuuza Tumbaku kwa Dola badala ya Shilingi ya Tanzania.

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**32. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, lini Serikali itajenga Uwanja wa Michezo wa kisasa Mkoani Njombe.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**33. MHESHIMIWA MWANTUM MZAMILU ZODO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, upi mkakati wa Serikali kukabiliana na vitendo vya ukatili vinavyoendelea nchini hasa kwa Wanawake na Watoto.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**34. MHESHIMIWA INNOCENT EDWARD KALOGERIS (MOROGORO KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itapeleka magari Vituo vya Polisi Kisaki na Mvuha ili kukabiliana na migogoro ya Wakulima na Wafugaji na kulinda raia na mali zao.

**35. MHESHIMIWA ASYA SHARIF OMAR (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itakarabati Nyumba za Makazi ya Polisi zilizopo Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

**WIZARA YA UJENZI:**

**36. MHESHIMIWA ATUPELE FREDY MWAKIBETE (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Zabuni ya Ujenzi wa Barabara ya Mbambo - Ntaba - hadi Ipinda kwa kiwango cha Lami itatangazwa.

**37. MHESHIMIWA MARY FRANCIS MASANJA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Nhungumalwa - Ngudu mpaka Magu kwa Kiwango cha lami.

**38. MHESHIMIWA STANSLAUS SHING'OMA MABULA (NYAMAGANA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaipandisha hadhi Barabara ya kutoka Mkolani Darajani - Nyakagwe hadi Busisi kwa kuiondoa TARURA na kuipeleka TANROADS.

**39. MHESHIMIWA HASSAN SELEMANI MTENGA (MTWARA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Kilambo.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka 2024.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **N.J. MWIHAMBI, *ndc*** |
| **28 AGOSTI, 2024** | **KATIBU WA BUNGE** |